

HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU  
WA MKOA WA RUKWA YA KUKABIDHI MRADI WA LISHE ENDELEVU  
TAREHE 25 JULAI, 2023

- **Katibu Tawala Mkoa,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**
- **Wakurugenzi wa Halmashauri,**
- **Makatibu Tawala Wilaya,**
- **Wakuu wa Seksheni na Vitengo Sekretarieti ya Mkoa,**
- **Wakuu wa Idara wa Halmashauri,**
- **Wadau wa Maendeleo (lishe endelevu),**
- **Wajumbe wa Timu ya uendeshaji wa huduma za Afya ya Mkoa na Halmashauri,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

Nawasalimu katika Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetukutanisha hapa tukiwa na afya njema. Vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati waandaaji wa Kikao hiki kwa kuona umuhimu wa kunikaribisha katika hafla hii ya Makabidhiano ya mradi ambapo nitakuwa kama Mwenyekiti ambaye nitasimamia makabidhiano ya Mradi huu, kutoka kwa Mdau – Lishe Endelevu kuja kwa Serikali. **Asanteni sana.**

**Ndugu washiriki**, Leo tunapokea Mradi kutoka kwa Ndugu zetu wa USAID/Lishe Endelevu, baada ya miaka mizuri mitano (5) ya kufanya shughuli zao katika jamii ya watu wa Rukwa. Waswahili wanasema, “lenye mwanzo halikosi mwisho”. Mlikusanyika kuufungua mradi huu na leo tumekusanyika tena kuufunga mradi, hongereni Lishe Endelevu – chini ya Mkurugenzi Mkuu wa Mradi Dr. Joyceline Kaganda. Hongera mtekelezaji Mama Save the Children International, na watekelezaji wenza PANITA, The Manoff Group, Delloite na AAPH bila kuwasahau IRDO.

**Ndugu washiriki**, Tunatambua Mchango wa Mradi huu katika Jamii yetu ya watu wa Rukwa, toka mwaka 2018 – 2023 mradi umekua ukiwahudumia watu wa Rukwa katika maeneo mbalimbali yenye kuleta matokeo chanya juu ya Lishe. Tumeona mambo mbalimbali yakifanywa na Mradi huu wa Lishe Endelevu katika Jamii yetu kama vile;:-

1. Kuwajengea uwezo watendaji wetu wa vijiji na Kata juu ya Mikataba ya Lishe na jinsi ya kuitekeleza – Kata zote 97.
2. Umewawezesha wakina mama vinara 113, ambao walikua viongozi wa kueneza elimu ya Lishe kwa jamii zao, kutokana na ushawishi walionao.
3. Umejengea uwezo kwa wahudumu 126 wa vituo vya Afya 109, katika kutoa Elimu bora ya Lishe kwa wateja.
4. Mradi umewawezesha Wahudumu wa afya ngazi ya Jamii 936, na kuwapa vitendea kazi kama vile baiskeli na mikoba kila mmoja.

5. Maafisa Kilimo 151, wakulima wa mfano 490 na wakulima wa kawaida 13,702 walifundishwa na kujengewa uwezo juu ya mbinu bora za kilimo ili kuongeza upatikanaji wa chakula.

**Ndugu washiriki**, Pia tumeona matokeo mengi mazuri chini ya ushirikiano bora na Lishe Endelevu, likiwemo la kuwa wa kwanza Kitaifa katika kutekeleza Mkataba wa Lishe kwa mwaka 2022. Hali ya lishe imekua ikiimarika katika jamii zetu kwa sababu ya kuongezeka kwa ufahamu juu ya Lishe, kuongezeka kwa uzalishaji na mabadiliko ya tabia juu ya Lishe.

**Ndugu Washiriki**, Kabla ya kuhitimisha, ninaomba sana kwetu tunaokabidhiwa mradi kuhakikisha kuwa mradi unakuwa endelevu. Mradi ulikuwepo kutusaidia, na uzuri tulifanya kazi wote tukishirikiana, kwa hiyo itasikitisha kama shughuli tunazokabidhiwa leo zitakufa baada ya miezi michache.

Baada ya kusema haya naomba nitamke kuwa tunapokea Mradi wa Lishe Endelevu. “Kazi lendele”.

**Mungu Ibariki Tanzania,**

**Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,**

Asanteni sana kwa kunisikiliza

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA**